

Wito wa Huduma Baada ya Kubakwa

KILA SAA
INAYOPITA
NI MUHIMU
Kasi ni Lazima.



Je, unajua kila saa inayopita baada ya kubakwa ni muhimu sana?

Kampeni ya Kila Saa ni Muhimu inalenga kuhamasisha zaidi kuhusu umuhimu mkubwa wa kupata kwa haraka huduma inayohitajika baada ya kubakwa, na inatoa wito kwa viongozi wa kitaifa na kijamii kuhakikisha huduma maridhawa zinapatikana katika jamii zote.

Watu wengi hawana habari kuhusu huduma nyingi zinazoweza kusaidia waathirika kupona kiwewe kinachotokana na kubakwa. Waathirika wana masaa 72 kupata matibabu ya kuzuia maambukizi ya virusi vya ukimwi, na masaa 120 kupata matibabu ya dharura ya kuzuia mimba. Na pia kwa kutegemea mazingira, matibabu ya haraka ya kiwewe yanaweza kuzuia athari zingine za kiafya za kipindi kifupi, na kipindi kirefu. Msaada wa afya ya kiakili pia ni muhimu sana, ingawa hilo linaweza kufanyika wakati wowote.

Ukatili wa kingono ni ukiukwaji wa haki za binadamu na ni tatizo lililoenea sana ulimwenguni dhidi ya watu wazima na watoto. Inakadiriwa mwanamke mmoja kati ya kila wanawake watatu duniani amefanyiwa ukatili kimwili au unyanyasaji wa kingono. Katika kila nchi ambako uchunguzi kuhusu dhuluma dhidi ya watoto umefanyika, inakadiriwa asilimia 25 ya wasichana walishiriki ngono kwa mara ya kwanza kwa kulazimishwa, na kwa walio wengi, ilitokea kabla hawajafikisha umri wa miaka 16. Nchini Marekani, inakadiriwa asilimia 11 ya wasichana wa shule za upili wanaripoti kuwa wamebakwa. Visa vingi vya ubakaji, pasipo kuzingatia mazingira, haviripotiwi. Kwa mfano, uchunguzi kuhusu ukatili dhidi ya watoto ulibaini kuwa idadi ya wavulana na wasichana waliopata huduma za kuwasaidia baada ya kunyanyaswa kingono haifiki asilimia 5 ya idadi ya watoto wote waliotendewa ukatili huo.

Je, kwa nini ni waathirika wachache mno wanaopata msaada wanaouhitaji? Wengi hawajui kila saa inayopita ni muhimu. Katika sehemu nyingi duniani, hakuna huduma ya kuwatunza waathirika, na inakopatikana watu wanaweza wasijue ni wapi wanaweza kuipata.

Hata pale ambapo huduma zinapatikana, unyanyapaa na hali ya kujilaumu inawafanya waathirika wengi wasiende kupata huduma hiyo. Matatizo hayo yote yanakuwa makubwa zaidi kwa watoto.

Ni jukumu letu kuchukua hatua ili waathirika waweze kuzungumza, kupata kutunzwa, na kupona. **Ndio sababu sisi tuliotia sahihi waraka huu tunatoa wito kwa serikali za kitaifa, mashirika, na jamii kote duniani kufanya hivi:**

1. Kuhakikisha huduma maridhawa za kuwasaidia waathirika baada ya kubakwa zinapatikana katika kila jamii, mkiwemo watoto;
2. Kuhamasisha watu kuhusu faida za kupata haraka huduma ya kiafya punde baada ya kubakwa, na kuelimisha jamii kuhusu huduma hizo zinapatikana wapi;
3. Kupunguza vihunzi vinavyokwamisha upatikanaji wa huduma za kuwatunza waathirika, kwa kubuni sera zinazowasaidia waathirika;
4. Kujenga mazingira ya kujisikia salama kuzungumza kuhusu ubakaji na kuhakikisha waathirika wanapata haki, na sheria itekelezwe dhidi ya wahalifu wanaobaka; na
5. Kuwekeza katika kukomesha aina zote za ukatili wa kingono.

Ili kujiunga na kampeni hii, tembelea everyhourmatters.org.

TOGETHER FOR GIRLS GLOBAL PARTNERS:



EVERY HOUR MATTERS PARTNERS:



FOR MORE INFORMATION VISIT: WWW.EVERYHOURMATTERS.ORG / WWW.TOGETHERFORGIRLS.ORG